# JARIDA LA USHIRIKA

ISSN 2714 - 2175 Toleo Na: 005 Januari - Machi, 2021




## "HAKIKISHENI VITENDEA KAZI HIVI VINATUNZWA NA KUTUMIKA VIZURI ILI KUFIKIA MALENGO YALIYOKUSUDIWA" – WAZIRI WA KILIMO





*"Ushirika - Pamoja Tujenge Uchumi Imara na Endelevu"*

# SALAMU ZA PONGEZI









# YALIYOMO


| | |
|---|---|
| KUTOKA KWA MRAJIS NA MTENDAJI MKUU WA TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA | 04 |
| WAZIRI WA KILIMO AKABIDHI MAGARI NA KOMPYUTA KWA WARAJIS WASAIDIZI WA MIKOA | 05 |
| TAFITI ZA USHIRIKA KULETA SULUHU YA CHANGAMOTO ZA USHIRIKA | 07 |
| MCHANGO WA USHIRIKA WA KILIMO KWENYE MAENDELEO YA VIWANDA NCHINI | 09 |
| SERIKALI YADHAMIRIA KUREJESHA HESHIMA NA HADHI YA USHIRIKA NCHINI | 11 |
| ZIJUE KAGUZI ZA VYAMA VYA USHIRIKA | 13 |
| SHERIA YA USHIRIKA KUFANYIWA MAPITIO | 15 |
| USHIRIKA MKOMBOZI WA WANAWAKE | 16 |
| MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE KATIKA PICHA | 18 |
| WAJUMBE WAPYA WA BODI ZA VYAMA WAPIGWA MSASA NA KULA KIAPO | 19 |
| MASWALI NA MAJIBU KUHUSU CHAGUZI ZA VIONGOZI WA VYAMA VYA USHIRIKA | 21 |
| MCHANGO WA VYAMA VYA USHIRIKA WA NYUMBA KUFIKIA AZMA YA NYUMBA KWA WOTE | 22 |
| MIFUMO YA KIMASOKO YAWANUFAISHA WAKULIMA WA MKOA WA RUVUMA NA KUWAWEZESHA KUPATA BILIONI 28.6 | 24 |
| WAKULIMA WA CHOROKO MWANZA WANUFAIKA NA MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA | 26 |

# KUTOKA KWA MRAJIS NA MTENDAJI MKUU WA TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA

## - Tumekusudia Kuimarisha Usimamizi wa Ushirika

SERIKALI imekusudia kuendeleza na kuimarisha Vyama vya Ushirika nchini ili kuleta tija kwa Wananchi na hatimaye kuijenga Tanzania yenye uchumi wa kati na wa viwanda kupitia Vyama vya Ushirika.

Nina imani kubwa kuwa Ushirika ukiendeshwa na kusimamiwa vizuri unayo fursa kubwa ya kushiriki katika kujenga, kuimarisha na kustawisha uchumi wa nchi yetu na maisha ya wananchi kwa ujumla.

Kupitia Dira ya Maendeleo ya Taifa, Serikali imeweka mikakati mbalimbali ya kuinua uchumi wa Wananchi na Taifa kwa ujumla. Serikali imekuwa ikitekeleza mipango mbalimbali ili kufanikisha malengo ya kitaifa tuliyojiwekea. Katika kuimarisha utendaji wa Watumishi walioko katika Sekta ya Ushirika Serikali imeamua kununua vitendea kazi, ili kuongeza usimamizi wa vyama kwa lengo la kuongeza ufanisi kwenye Vyama na kuwanufaisha Wananchi kiuchumi ambalo ni lengo moja wapo la Taifa. Vitendea kazi hivyo ikiwa ni pamoja na Magari na kompyuta zilizonunuliwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, pamoja na kompyuta zilizotolewa na Benki ya CRDB ni nyenzo muhimu zitakazosaidia kutufikisha tunakoelekea katika kuimarisha Sekta ya Ushirika nchini. Magari yatasaidia kupunguza tatizo la usafiri kwa Warajis Wasaidizi na Maafisa Ushirika wanaosimamia Vyama vya Ushirika huko Mikoani na kompyuta zitasaidia kuimarisha matumizi sahihi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Teknolojia hii itawezesha kupunguza na kuondoa changamoto mbalimbali zilizokuwa zikijitokeza; ikiwemo ucheleweshaji wa kazi kwenye uandikishaji wa Vyama vya Ushirika, upotevu wa kumbukumbu na utunzaji duni wa takwimu katika Sekta ya Ushirika.



*Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dkt. Benson Ndiege*

Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo inaahidi kuendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa Watumishi wa Sekta hii muhimu kwa Maendeleo ya Wananchi na Taifa kwa ujumla. Tutaendelea kununua magari zaidi na kuongeza vitendea kazi vingine ili kuimarisha usimamizi wa Sekta ya Ushirika nchini.

Tume ya Maendeleo ya Ushirika tukiwa wasimamizi wa Vyama vya Ushirika nchini, tunaahidi kutekeleza ipasavyo Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025 ambayo imetoa Maelekezo mahsusi ya kutekelezwa katika Sekta ya Ushirika. Maelekezo yaliyotolewa ni: ***"Katika kipindi cha miaka mitano (2020 - 2025), Chama Cha Mapinduzi kitahakikisha dhana ya Ushirika wa hiari inajengwa na kusimamiwa na sheria ili kuwalinda na kuwanufaisha wanaushirika, hivyo kuchangia ipasavyo katika ustawi wao na Taifa kwa ujumla"***

# WAZIRI WA KILIMO AKABIDHI MAGARI NA KOMPYUTA KWA WARAJIS WASAIDIZI WA MIKOA




*Waziri wa Kilimo, Profesa Adolf Mkenda akikabidhi gari aina ya Nissan Hard Top N 300 Double Cabin 4WD kwa Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoa wa Njombe, Consolatha Kiluma (kushoto).*

Waziri wa Kilimo, Profesa Adolf Mkenda, mwezi Januari 2021 amekabidhi magari manne aina ya Nissan Hard Top N 300 Double Cabin 4WD yenye jumla ya thamani ya Shilingi 275,091,670/- kwa Warajis Wasaidizi wa Vyama vya Ushirika wa Mikoa minne. Mikoa hiyo ni Simiyu, Kilimanjaro, Njombe na Dar es Salaam. Aidha, gari moja lililokuwa likitumika makao makuu ya Tume limepelekwa kuhudumia Mkoa wa Kigoma ili kusaidia mpango wa Serikali wa kuimarisha zao la Mchikichi.

Waziri wa Kilimo Prof. Mkenda pia amekabidhi kompyuta 25 pamoja na printa moja (1) zenye jumla ya thamani ya Shilingi 49,050,000/-. Akizungumza na Washiriki wa hafla ya makabidhiano, Waziri Mkenda amesema magari na kompyuta alizowakabidhi Warajis Wasaidizi zikatumike kuongeza kasi ya uwajibikaji kwa Watumishi walioko katika maeneo mbalimbali nchini ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Waziri Mkenda amesema vitendea kazi hivi ni kwa ajili ya kuimarisha shughuli za utendaji kwa lengo la kuboresha kasi ya utendaji kazi kwenye usimamizi wa Vyama vya Ushirika.

"Hakikisheni vitendea kazi hivi vinatunzwa ipasavyo na kutumika vizuri ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Aidha, naagiza Ofisi ya Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika isimamie ipasavyo matumizi na matunzo ya vifaa hivi kwa kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara," amesema Waziri Mkenda.

“Kwa kuwa ninyi ni wasimamizi wa Vyama vya Ushirika katika ngazi ya Mikoa, nawaagiza kutekeleza ipasavyo Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025 ambayo imetoa maelekezo mahsusi ya kutekelezwa katika Sekta ya Ushirika.” Amesema Prof. Mkenda.

Waziri Mkenda amewataka Warajis Wasaidizi wa Mikoa kuisoma na kuielewa Ilani ya Chama Tawala, hasa Aya ya 34 inayosema: ‘Katika kipindi cha miaka mitano (2020 - 2025), Chama Cha Mapinduzi kitahakikisha dhana ya Ushirika wa hiari inajengwa na kusimamiwa na sheria ili kuwalinda na kuwanufaisha Wanaushirika, hivyo kuchangia ipasavyo katika ustawi wao na Taifa kwa ujumla’. Amesema kuwa wakati wote Warajis wa Mikoa wawe tayari kutoa taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya CCM katika maeneo yao kwenye ngazi ya Mikoa na Wilaya zao.

Profesa Mkenda amempongeza Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania kwa kukusanya mapato ya Tume na kununua magari manne yenye thamani ya shilingi 275.

“Ninafahamu kuwa vitendea kazi ninavyowakabidhi leo ikiwemo magari kwa ajili ya usafiri wa Watumishi katika kutekeleza majukumu yao havitatosheleza kwa wote; magari haya manne (4) yanakabidhiwa kwa Mikoa minne (4) na gari moja lililokuwa likitumika makao makuu ya Tume litakwenda kuhudumia mkoa wa Kigoma. Hivyo, jumla ya mikoa saba (7) itakuwa na magari ikiwemo mikoa ya Mtwara na Tabora,” alisema Prof. Mkenda.

“Hivyo basi, jumla ya mikoa ishirini (20) bado itabakia kuwa haina magari. Naomba niwahakikishie kuwa Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa maendeleo itaendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa Watumishi wa Sekta hii muhimu kwa kuendelea kununua magari zaidi na kuongeza vitendea kazi vingine ili kuimarisha usimamizi wa Ushirika nchini.” amesema Prof. Mkenda.

Akizungumza katika Hafla hiyo, Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dkt. Benson Ndiege, amesema Tume imenunua magari mapya manne (4) aina ya Nissan Double Cabin 4WD yenye jumla ya thamani ya Shilingi 275,091,670/-. Pia Tume imenunua kompyuta 25 pamoja na printa moja (1) zenye thamani ya Shilingi 49,050,000/- kwa ujumla; Vilevile, Tume imekabidhiwa na Benki ya CRDB jumla ya kompyuta 50 ili kurahisisha shughuli za utendaji wa majukumu yake.



*Warajis Wasaidizi wa Mikoa Tanzania Bara mara baada ya kukabidhiwa kompyuta mpakato na Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, mwezi Januari 2021, Jijini Dodoma*




*Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo Prof. Siza Tumbo akifungua Kongamano la Kwanza la Tafiti za Ushirika, Jijini Dodoma*

# TAFITI ZA USHIRIKA KULETA SULUHU YA CHANGAMOTO ZA USHIRIKA

Tafiti za Ushirika zikitumika ipasavyo zimetajwa kuwa zinaenda kuongeza kasi na chachu ya maendeleo katika utatuzi wa Changamoto zilizopo katika Sekta ya Ushirika nchini.

Hayo yamesemwa na Naibu Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Prof. Siza Tumbo, akifungua Kongamano la Kwanza la Tafiti za Ushirika linalofanyika kuanzia Machi 16 -18, 2021, Jijini Dodoma.



*Dkt. Audax Rutabanzibwa Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi akifafanua jambo wakati wa Kongamano la Kwanza la Tafiti za Ushirika, Jijini Dodoma*

Akifungua Kongamano hilo Naibu Katibu Mkuu ameeleza Tafiti mbalimbali zinazofanywa na Taasisi pamoja na Wadau kwa sasa bado hazijatumika ipasavyo kwani nyingi zimekuwa zikichapishwa na pengine kuhifadhiwa kwenye maktaba tu. Hivyo, kutofahamika na kuwanufaisha wanachama na wadau katika Sekta ya Ushirika.

"Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa Vyama vya Ushirika vinanufaika na matokeo ya Tafiti zinazofanywa na wadau mbalimbali ili kuinua utendaji na kuondoa changamoto zinazoikabili Sekta ya Ushirika," alisema Naibu Katibu Mkuu

Akieleza Malengo ya Kongamano hilo Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dkt. Benson Ndiege, amesema Kongamano la Tafiti za Ushirika linalenga kuwakutanisha wadau, watafiti na wanaushirika ili kujadili namna bora ya kuboresha Sekta ya Ushirika kupitia tafiti zinazofanyika kupitia



***Washiriki wa Kongamano la Kwanza la Tafiti za Ushirika wakifuatilia majadiliano katika Kongamano, Jijini Dodoma***

maoni na mapendekezo yanayotolewa pamoja na uzoefu katika Sekta ya Ushirika.

Dkt. Benson Ndiege amezitaja baadhi ya Changamoto zinazoikabili Sekta hiyo ni pamoja na Ushirika kutokidhi mahitaji ya Wanachama, ukosefu wa mitaji, uongozi mbovu, ubadhilifu na elimu duni ya Ushirika.Aliongeza kuwa ni wakati muafaka sasa kwa wadau wote wa Ushirika kushirikiana kwa pamoja kutatua changamoto za Ushirika ili kuimarisha na kuongeza kasi ya maendeleo ya Ushirika.

Aidha, Mrajis amefafanua kuwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika ina malengo makuu ya kuhakikisha kuwa Wanachama wa Ushirika wanakuwa na uelewa pamoja na uweledi wa kutosha katika Ushirika, uongozi na uwajibikaji katika Vyama vya Ushirika, kuwa na Vyama vya Ushirika imara na Vyama vya kifedha (SACCOS) kuwa na mitaji imara.

Kwa upande wake Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, Prof. Alred Sife katika hotuba yake iliyosomwa na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, Taaluma, Prof. John Safari, amesema ni matarajio ya Chuo kuwa, Makongamano ya Tafiti za Ushirika yatasaidia kuongeza uelewa wa vikwazo vya maendeleo ya Ushirika, Kujenga Ushirika unaoendana na mabadiliko ya kijamii na kiuchumi na kufanya Sekta ya Ushirika kuwa msingi imara wa Uchumi wa Taifa nchini.




***Naibu Katibu wa Wizara ya Kilimo, Prof. Siza Tumbo (wa tatu kushoto waliokaa) akiwa na viongozi kutoka Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi pamoja na Kamati ya Maandalizi ya Kongamano la kwanza la Tafiti za Ushirika, Jijini Dodoma***

# MCHANGO WA USHIRIKA WA KILIMO KWENYE MAENDELEO YA VIWANDA NCHINI

**Ushirika wa kilimo ambao pia unajulikana kama Ushirika wa Kilimo na Masoko ni ushirika ambao wakulima hujumuisha rasilimali zao katika maeneo fulani ya shughuli na kuzitumia kwa pamoja kwa ajili ya kuongeza tija kwenye zao linalozalishwa na ushirika huo.**

Ushirika wa Kilimo unaweza kujikita katika kuzalisha,kukusanya,kuchakata (kuongeza thamani) na kutafuta masoko. Katika hatua ya kuzalisha kwenye Vyama vya Ushirika,Viongozi huhakikishia Wanachama kupata pembejeo bora za uzalishaji kwa wakati na kwa bei nafuu. Aidha, wakati wa masoko, Wanachama hukusanya pamoja na kukubaliana bei itakayomfaidisha Mkulima baada ya kuangalia gharama za uzalishaji wa zao hilo.

Dira ya Maendeleo ya Taifa, 2025 inaelezea azma ya Nerikali kuwa nchi yenye viwanda vingi ambavyo vitakuwa na mchango katika uchumi wa Taifa na kufikia kiwango cha chini cha 40% ya Pato la Taifa. Katika mwaka 2016/2017 viwanda vingi vikubwa na vidogo vilijengwa nchini ambapo vilisaidia kutengeneza ajira na kukuza uchumi wa Nchi. Hata hivyo, viwanda vingi vimejengwa na vingine kufufuliwa katika Vyama vya Ushirika wa mazao kwa lengo la kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa na Wanachama wa vyama hivyo ili kuongeza tija kwa Mkulima.



***Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (wa pili kulia) akikagua sehemu ya mitambo ya kiwanda cha kuchakata pamba cha Manawa kilichopo mkoani Mwanza, kinachomilikiwa na Chama Kikuu cha Ushirika Nyanza - NCU.***



***Mfanyakazi katika Kiwanda cha kusindika mkonge akiwa katika uandaaji wa Katani katika mtambo wa Korona kilichopo Wilaya ya Korogwe Mkoani Tanga***

Vyama vya Ushirika vya mazao vina uwezo wa kuwa na viwanda vingi kuliko Taasisi nyingine yoyote kutokana na kwamba zaidi ya asilimia 70 ya mali ghafi za viwanda zinazalishwa na kuuzwa kupitia vyama vya ushirika. Kwa mfano mazao ya Korosho, Pamba, Tumbaku, Chai, Mkonge na Kahawa yanazalishwa na kuuzwa kupitia mfumo wa Vyama vya Ushirika.

Kwa mantiki hiyo, Tanzania ina mtandao mzuri wa Vyama vya Ushirika kote nchini unaofaa kuongoza mchakato wa viwanda, kinachokosekana mara nyingi ni utashi wa kisiasa kutumia mtandao wa Vyama vya Ushirika ili kuwezesha uratibu na utekelezaji. Vyama vya Ushirika ni taasisi zinazoweza kutafsiri nia ya Serikali ya viwanda kwa uwazi au dhahiri na kwa vitendo.

Vyama vya Ushirika wa mazao vinatakiwa kuchakata mazao yanayozalishwa na wakulima kwa kuongeza mnyororo wa thamani kupitia viwanda vya Ushirika ili kumnufaisha Mkulima kwa kumwezesha kupata bei nzuri ya mazao yake na kuongeza ajira. Haya kwa sasa yanafanyika katika zao la Pamba ambapo kwa msimu wa 2020/2021 Vyama Vikuu vya Ushirika Kahama na Chato vimekusanya na kuchakata Pamba ya Wanachama wake kupitia viwanda vya chama na kuiuza kwa bei nzuri. Kwa miaka mingi Pamba iliyokuwa ikizalishwa kupitia Vyama vya Ushirika ilikuwa ikiuzwa ikiwa ghafi ambapo Wanunuzi walikuwa wakiinunua kwa bei ya chini ambayo ilikuwa ikimnyonya Mkulima. Katika misimu inayoendelea, Pamba ya Mwanachama inaweza kuchakatwa na kupata bidhaa zaidi ya moja ambazo zote zinampa Mwanachama faida kama vile mbegu za mafuta, mashudu n.k.

Tume ya Maendeleo ya Ushirika inaendelea na juhudi za kufufua viwanda vya Ushirika kwa lengo la kuongeza mapato ya Vyama vya Ushirika na kumnufaisha Mkulima. Aidha, Vyama vya Ushirika vimetakiwa kuunga mkono jitihada za Serikali ambayo inaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuanzisha na kuendeleza Viwanda nchini. Jitihada hizo zinaenda sambamba na kuendelea kuhamasisha kilimo cha mazao ya kimkakati kama vile Pamba, Tumbaku, Kahawa, Chai na Korosho ili kuongeza malighafi zinazohitajika kwaajili ya viwanda.

# SERIKALI YADHAMIRIA KUREJESHA HESHIMA NA HADHI YA USHIRIKA NCHINI

- **Kuendelea Kuwabana Wezi na Wabadhirifu wa mali za Ushirika**



***Warajis Wasaidizi wa Vyama vya Ushirika Tanzania Bara wakimsikiliza Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda (hayupo pichani) Jijini Dodoma, Januari 2021***

Waziri wa Kilimo, Profesa Adolf Mkenda, amewataka Wanaushirika kurejesha hadhi na heshima ya Ushirika nchini kwa kujenga imani ya Wananchi kwenye Sekta hiyo na kuimarisha vyama vya ushirika ili viweze kuleta tija kwa wanachama na hatimaye kuijenga Tanzania yenye uchumi imara kupitia Vyama vya Ushirika.

Prof. Mkenda alikuwa akizungumza kwenye Hafla ya Kukabidhi Vitendea Kazi kwa Warajis Wasaidizi wa Vyama Vya Ushirika wa Mikoa, iliyofanyika Jijini Dodoma, mwezi Januari, 2021 ambapo ameitaka Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) kwa kushirikiana na wadau wengine wa Ushirika kurudisha Imani ya wananchi kwenye Ushirika.

"Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kurudisha Imani ya wananchi kwenye Vyama vya Ushirika, kwa kuhakikisha dhana ya Ushirika wa hiari inajengwa na kusimamiwa na Sheria ili kuwalinda na kuwanufaisha wanaushirika, hivyo kuchangia ipasavyo katika ustawi wao na Taifa kwa ujumla," amesema Prof. Mkenda.

Waziri wa Kilimo amesema kuwa Serikali katika kuimarisha Ushirika inafanya Mapitio ya Sheria ya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013 ili kuondoa mapungufu yaliyokuwa yanajitokeza katika utekelezaji wa shughuli za ushirika nchini. Aidha, Serikali itaendelea kupambana na wizi na ubadhirifu unaojitokeza kwenye Vyama vya Ushirika.

**"Hatutachekeana na wezi na wabadhirifu wanaovihujumu Vyama vya Ushirika, tutapambana nao**

**ili mali ya Wanaushirika iwe salama na iwanufaishe katika kujiletea maendeleo waliyokusudia. Hata hivyo, Serikali haitaviingilia Vyama vya Ushirika vinavyofuata Sheria, Miongozo na Taratibu zilizowekwa katika uendeshaji wake,"** amesema Prof. Mkenda.

Waziri Mkenda amesema kuwa Serikali haitakubali kuona mtu anacheza na mali za ushirika, kwasababu ikifanya hivyo, itakatisha watu tamaa na watakuwa hawana mwamko wa kujiunga na Ushirika.

Alisema bado kunahitajika mapambano dhidi ya wizi na ubadhirifu kwenye Vyama vya Ushirika licha ya kuonekana kupungua kutokana na jitihada zilizofanywa na Serikali za kurudisha mali za Ushirika. Alisema kuwa licha ya ubadhirifu kupungua, bado kuna tatizo la vyama kushindwa kuandaa vyema hesabu zake na kusababisha kukosa Hati Safi.

"Kuna kazi kubwa ya kujenga uwezo, kuna Ripoti ya COASCO, ukiisoma inaonekana mbaya sana, lakini kwa kiasi fulani inaonyesha ni udhaifu, ambapo ripoti inaanisha kuwa katika vyama vilivyokaguliwa hakuna mhasibu mzuri anayeweza kuandaa vitabu vya hesabu ambavyo vitakaguliwa," alisema Waziri Mkenda.

Ripoti ya Ukaguzi wa vyama vya ushirika uliofanywa na Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) kwa mwaka 2019/20, inaonyesha kuwa katika vyama vikuu 43 vilivyokaguliwa hakuna chama kilichopata Hati Safi.

Vilevile, alisema Ripoti hiyo inaonyesha kuna tatizo la kutokuweka vizuri kumbukumbu na kwa uchache kuna wizi na ubadhirifu. Hivyo, kuna haja ya kujenga uwezo wa kuweka kumbukumbu ili kuviwezesha Vyama kupata Hati Safi.

**"Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kurudisha Imani ya wananchi kwenye Vyama vya Ushirika, kwa kuhakikisha dhana ya Ushirika wa hiari inajengwa na kusimamiwa na Sheria ili kuwalinda na kuwanufaisha wanaushirika, hivyo kuchangia ipasavyo katika ustawi wao na Taifa kwa ujumla,"**

# ZIJUE KAGUZI ZA VYAMA VYA USHIRIKA

## 1.0 MAANA YA UKAGUZI

Ukaguzi wa Chama cha Ushirika maana yake ni kuchunguza vitabu vya hesabu, hati, mali, dhima na kumbukumbu nyingine zinazotunzwa na Chama hicho ili kuona kuwa uendeshaji wa shughuli za Chama hicho unazingatia maamuzi ya wanachama, masharti ya Chama, Sheria na Kanuni za Vyama vya Ushirika pamoja na Sheria zingine za nchi.

### 1.1 Madhumuni ya Ukaguzi

Madhumuni ya Ukaguzi wa Chama cha Ushirika ni:

- Kufuatilia maendeleo ya shughuli za Chama,
- Kuona udhibiti wa hali ya fedha na mali nyingine za Chama,
- Kuthibitisha kuwa vitabu vya hesabu, nyaraka na kumbukumbu zote zinaandikwa na kutunzwa ipasavyo,
- Kubaini mapato na matumizi ya Chama kwa kuzingatia makisio ya mapato na matumizi yaliyoidhinishwa na Mrajis, na
- Kutoa ushauri juu ya uendeshaji wa shughuli za Uchumi na Uongozi.

## 2.0 AINA ZA UKAGUZI:

- Ukaguzi wa mara kwa mara (Continuous inspection)
- Ukaguzi wa dharura (Surprise check/ inspection)
- Ukaguzi maalumu (Special Inspection or Investigation)
- Ukaguzi wa mwisho (Final Inspection)
- Ukaguzi wa nje (External Audit)

### 2.1 Ukaguzi wa Mara kwa Mara (Continuous Inspection)

- Katika aina hii ya Ukaguzi, Mkaguzi anatakiwa kuthibitisha kwamba vitabu vya hesabu na kumbukumbu zote za Chama zinaandikwa kwa usahihi na kwamba maelekezo yote ya Bodi ya Chama na yale ya Mikutano Mikuu yanatekelezwa.
- Kufuatana na Sheria ya Vyama vya Ushirika Namba 6 ya mwaka 2013, Mrajis wa Vyama vya Ushirika amepewa uwezo wa kuamua kufanyika kwa Ukaguzi wa mara kwa mara
- Moja ya madhumuni ya Ukaguzi huu, ni ufuatiliaji wa maendeleo ya shughuli za Chama, Udhibiti wa fedha na mali zingine katika vipindi tofauti vya Ukaguzi ndani ya mwaka wa fedha wa Chama.

### 1.2 Ukaguzi wa Dharura (Surprise Check/Inspection)

- Ukaguzi huu hufanywa wakati wowote ndani ya mwaka wa fedha wa Chama.
- Ukaguzi wa dharura ni sawa na Ukaguzi wa mara kwa mara, kwa maana ya mchakato wa Ukaguzi wenyewe.
- Ukaguzi huu hufanywa kwa eneo fulani tu, mfano eneo la Mikopo, au eneo la akiba za Wanachama, pembejeo n.k. na hufanywa wakati wowote Mkaguzi anapoamua.

### 1.3 Ukaguzi Maalumu (Special Inspection or Investigation)

- Madhumuni ya Ukaguzi huu ni kuthibitisha ukweli ama uongo wa tuhuma/malalamiko yoyote kuhusu Chama cha Ushirika.
- Ukaguzi huu unakuwa wa eneo tu kama ilivyo kwenye Ukaguzi wa dharura.

## 2.4 Ukaguzi wa Mwisho (Final Audit)

- Ukaguzi wa Mwisho unafanyika mwisho wa mwaka wa hesabu za Chama.
- Madhumuni ya Ukaguzi huu ni kuchunguza vitabu vya hesabu vya Chama na kuandaa ripoti ambayo itakuwa ni msingi wa taarifa ya Maafisa Ushirika kwa Wanachama.
- Wakati huo huo Ukaguzi huu unahakikisha kwamba vitabu vyote na kumbukumbu nyinginezo zinakuwa sahihi kwa ajili ya Wakaguzi wa Nje (External Auditors).

## 2.5 Ukaguzi wa Nje (External Audit)

- Ukaguzi wa Nje unafanyika mwisho wa mwaka wa Fedha wa Chama.
- Ukaguzi wa Nje hufanywa na Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) au Kampuni yoyote ya Ukaguzi iliyopitishwa na Mkutano Mkuu wa chama na kupewa kibali na Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

## 3.0 Hitimisho

Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika unaofanywa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika unajielekeza kuhakikisha kwamba

- Shughuli za Vyama zinaendeshwa kwa ufanisi na kwa manufaa ya Chama na Jamii
- Mali za Chama zinalindwa na kutumika kwa manufaa ya Wanachama na Jamii
- Hesabu za Chama zinaandikwa na kukaguliwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Ushirika
- Taarifa za Fedha, mapato na matumizi zinatolewa kila mwezi, robo, nusu mwaka na kuhakikisha zinajadiliwa kwa uwazi mbele ya Bodi na Wanachama
- Taarifa za ukaguzi zinasomwa kwenye Mkutano Mkuu wa Chama

# SHERIA YA USHIRIKA KUFANYIWA MAPITIO

**Wizara ya Kilimo inajipanga kuanza kupitia upya Sheria ya Ushirika na kupata maoni ya wadau ili kuwa na sheria mpya ya Ushirika itakayoendana na mazingira ya sasa.**

Kauli hiyo ilitolewa na Waziri wa Kilimo, Profesa Adolf Mkenda wakati akiongea na Watumishi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) na Wadau wa Ushirika Jijini Dodoma mapema mwezi Januari, 2021.

Alisema upitiaji huo ni sehemu ya mikakati ya wizara kuhakikisha heshima na hadhi ya Sekta ya Ushirika inarejeshwa kama ilivyokuwa miaka ya mwanzoni mwa uhuru wa Tanzania Bara ambapo Ushirika uliweza kujiendesha na kuchangia zaidi kwenye ukuaji wa uchumi.

"Kuna maendeleo makubwa kwenye Ushirika lakini tuna kazi ya kuhakikisha tunarudisha heshima na hadhi ya ushirika wenye uwezo na nguvu ya kutafuta masoko ya mazao ya wakulima na kuchangia zaidi kwenye ukuaji wa uchumi kama ilivyokuwa miaka ya 1950" alisema Prof. Mkenda

Waziri Mkenda alisema pia nia ya wizara yake ni kudhibiti wizi na ubadhirifu wa mali za wanaushirika ambapo amepongeza kazi nzuri iliyofanywa na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa kupitia Kamati Maalumu ya kufuatilia na kurejesha mali za ushirika zilizokuwa zimeporwa na kuuzwa kinyume cha utaratibu na sheria.

Aidha, alisema wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika itawajengea uwezo watumishi wake ili waweze kuratibu na kusimamia sekta ya ushirika kwa weledi zaidi.




***Waziri wa Kilimo, Profesa Adolf Mkenda, akiongea na Watumishi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) na Wadau wa Ushirika Jijini Dodoma mapema mwezi Januari, 2021.***



*Mmiliki wa Shule ya watoto wadogo Cherish Daycare na Mwanachama wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo (UDOM SACCOS), CPA Ela Fute, akicheza kwa furaha na watoto shuleni Makulu, Dodoma*

# USHIRIKA MKOMBOZI WA WANAWAKE

Katika maeneo mbalimbali nchini Wanawake ndio msingi wa malezi ya Jamii zetu. Hii ni kutokana na majukumu na uwezo walionao katika kulea, kutunza familia na jamii zinazowazunguka.

Wanawake wengi walio katika harakati mbalimbali za kujikwamua kiuchumi wamekuwa wakijiunga na vikundi vinavyowaunganisha kwa lengo la kupata mitaji, masoko au uendeshaji wa miradi mbalimbali kama vile kilimo, biashara na shughuli nyingine za kiuchumi.

Katika Ushirika Wanawake wana fursa ya kuwa wanachama na viongozi wa Vyama vya Ushirika wa nyanja mbalimbali kutokana na Ushirika kuwa ni Sekta mtambuka yenye wigo mpana kiuchmi katika maeneo mengi ya nchi yenye Ushirika wa aina mbalimbali ikiwemo Kilimo, Uvuvi, Viwanda, Ufugaji, Nyumba na nyingine, zote zikiwezesha kutoa fursa nyingi kwa Wanawake kuchagua na kushiriki kulingana na nafasi, eneo, uwezo na maamuzi binafsi.

Katika mahojiano maalum ya Makala hii na Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Dkt. Benson Ndiege alieleza kuwa Wanawake wanaweza kunufaika na fursa za Ushirika kwa kujiunga kwa pamoja kuwa na nguvu ya pamoja katika kutafuta na kutumia fursa zinazowazunguka katika Nyanja mbalimbali.

Akizungumzia masuala ya Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) ambavyo vinapatikana maeneo mengi hapa nchini Dkt. Ndiege alibainisha kuwa Wanawake wanakutokana na upatikanaji wa Vyama hivi katika maeneo mengi nchini, masharti na vigezo nafuu vinavyoweza kuwasaidia Wanawake wengi kuanzisha biashara, mashamba, ujenzi na masuala mengi yenye kuongeza tija na maendeleo.

Akiongea kuhusu masuala ya Ufugaji na Wanawake, Meneja wa Chama cha Ushirika wa Wafugaji Ng'ombe wa Wilaya ya Korogwe (UWAKO), Zamuata Ismail ameeleza kuwa Chama hicho kina wanachama Wanawake ambao wanaendesha shughuli za Ufugaji Ngombe na kukusanya maziwa katika Chama hicho kwaajili ya kuwaunganisha wafugaji hao na Wanunuzi mbalimbali kwa uhakika wa soko la maziwa. Akifafanua zaidi kuwa wanunuzi wa

maziwa wanatoka ndani na wengine nje ya Wilaya ya Korogwe, mkoani Tanga.

Aidha, Meneja huyo ametoa wito kwa Wanawake na mabinti wengi hususani wanaomaliza masomo yao katika ngazi mbalimbali kwenye Vyuo na Taasisi nyingine za elimu kujishughulisha na Ufugaji katika maeneo yao na kujiunga na Vyama vya Ushirika ili kupata uhakika wa masoko na ushindani wa bei. Akiongeza kuwa Ushirika ni nyenzo muhimu inayowezesha kutosheleza na kufikia mahitaji makubwa ya masoko ambayo inaweza kuwa changamoto kwa mfugaji mmoja mmoja kutosheleza. Hivyo, nguvu ya pamoja kupitia Vyama vya Ushirika ni nyenzo muhimu kufikia mahitaji ya masoko.

"Wanawake wenzangu tusifikiri kuwa shughuli za Ufugaji ni za Wanaume pekee yake, tuingie kwenye ufugaji hasa wa Ngombe wa maziwa kwani Ufugaji ni zaidi ya biashara ukiweza kupata maziwa na uhakika wa soko kupitia Ushirika kama ilivyo hapa UWAKO kwa kweli tutafanikiwa kupunguza na hatimaye kuondokana na umaskini," alisema Meneja Zamuata.

Nae Meneja wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha kinachohudumia Wanawake wa Wilaya ya Karagwe na Kyerwa Mkoani Kagera (KAWOSA) Goliath Elias alieleza kuwa katika jitihada za kuwakwamua kiuchumi Wanawake hususani wa maeneo ya vijijini. KAWOSA ilianzisha programu ya kuwalipia karo za Shule watoto wenye mazingira magumu baadae wakabadili utaratibu na kutafuta mama wa watoto hao na kuwafundisha ujasiriamali mbalimbali na hatimaye kuanza kuwakopesha ili kuwawezesha wanawake hao kumudu na kuboresha hali za maisha yao.

Kwa upande wake CPA Ela Fute, mwanachama wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo UDOM SACCOS kilichopo Jijini Dodoma ambaye ni mmiliki wa Shule ya Awali ya watoto iitwayo Cherish Daycare and Nursery School amesema Mkopo kutoka Udom Saccos ulimwezesha kujenga madarasa, kununua gari kwa ajili ya watoto pamoja na kujenga nyumba yake ya makazi.

"SACCOS imenisaidia sana kwani awali sikuwa na madarasa nilianzia shule yangu na darasa mmoja nikiwa nimeanza na mtoto mmoja, nashukuru watoto wameongezeka na nimefanikiwa kuongeza madarasa ya watoto," alisema Fute

Dkt. Benson Ndiege Mrajis wa Vyama vya Ushirika aliainisha kuwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa mujibu wa Sheria Na. 6 ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2013 itaendelea kutekeleza jukumu la Kusimamia na kuhamasisha makundi mbalimbali ya Jamii wakiwemo Wanawake, Vijana na wenye Ulemavu kujiunga na kunufaika na fursa za Ushirika ili kujikwamua na kujiendeleza kiuchumi.



***Muonekano wa Shule ya watoto wadogo ya Cherish Day Care inayomilikiwa na mwanachama wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo UDOM SACCOS (CPA) Ela Fute, Makulu Dodoma.***

# MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE KATIKA PICHA




***Watumishi Wanawake wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika katika Picha ya Pamoja wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, Jijini Dodoma***



***Wanawake wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika wakiwa pamoja na wanafunzi wa Shule ya msingi Buigiri baada ya kukabidhi mahitaji mbalimbali katika Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani Machi 8,2021.***



***Baadhi ya Wanawake wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika wakikabidhi mahitaji kwa wanafunzi wa Shule ya msingi Buigiri wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani Machi 8, 2021.***

# WAJUMBE WAPYA WA BODI ZA VYAMA WAPIGWA MSASA NA KULA KIAPO

Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu Endelevu ya Ushirika kutoka Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Dkt. Gervas Machimu, ameipongeza Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) kwa kuzingatia Sheria ya Vyama vya Ushirika inayoelekeza Mrajis wa Vyama vya Ushirika kutoa Mafunzo kwa Viongozi wapya waliochaguliwa na kuwaomba Viongozi wote walioshiriki mafunzo hayo washiriki kwa ukamilifu kwaajili ya kuleta mabadiliko kwenye Vyama vyao.

Dkt. Machimu ameyasema hayo wakati akifungua mafunzo kwa Viongozi Wapya wa Bodi za Uongozi na Kamati za Usimamizi wa Vyama Vya Ushirika mkoani Kilimanjaro yaliyofunguliwa Februari 16, 2021 katika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kilimanjaro.

Aidha, Dkt. Machimu ametoa wito kwa viongozi wa Bodi na Kamati ya Usimamizi kuwaajiri Watendaji wenye taaluma ya uendeshaji wa Vyama vya Ushirika kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi wa utendaji kwenye Vyama. Akiongeza kuwa ni muhimu kutumia Taasisi ya Elimu ya Juu kutoka Chuo cha Ushirika kujiendeleza kupitia Kozi mbalimbali za Ushirika.

Mratibu wa Mafunzo hayo, Mkurugenzi wa Utafiti na Mafunzo kutoka Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Bi. Doroth Kalikamo, aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kuzingatia Historia ya Ushirika, Misingi ya Ushirika pamoja na Madhumuni ya Vyama vya Ushirika.



**Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu Endelevu ya Ushirika kutoka Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU),** ***Dkt. Gervas Machimu (wa sita kushoto, msitari wa mbele) akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa Mafunzo ya Viongozi Wapya wa Bodi za Uongozi na Kamati za Usimamizi wa Vyama Vya Ushirika mkoani Kilimanjaro***



*Viongozi Wapya wa Bodi za Uongozi na Kamati za Usimamizi wa Vyama Vya Ushirika wakiwa katika mafunzo elekezi Mkoani Kilimanjaro*

"Ni vizuri sisi kama viongozi wa Vyama vya Ushirika tukaitambua Historia ya Ushirika, Chimbuko lake, Changamoto ulizopitia, Misingi ya ushirika, Sheria na Kanuni zake pamoja na Madhumuni ya ushirika," alisema Kalikamo.

Kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Wajumbe wa Bodi na Viongozi wa Vyama kujaza Fomu za Tamko la Mali na Madeni ikifuatiwa na hatua ya viapo vya uadilifu.

Mkoani Tanga, Wajumbe wapya wa Bodi za Vyama vya Ushirika toka Halmashauri ya Korogwe DC, Korogwe Mji na Handeni DC walipatiwa Mafunzo ya namna ya kusimamia Vyama vya Ushirika na mwisho wa Mafunzo hayo walikula kiapo cha Uadilifu. Mafunzo hayo yaliyofanyika Machi, 2021 yaliyosimamiwa na Ofisi ya Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoa wa Tanga, Jackline Senzighe.

Mafunzo hayo yalihusisha wawezeshaji kutoka Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) - Tanga, Ofisi ya Mrajis Msaidizi (M) Tanga na Mkaguzi kutoka COASCO Tanga kwa lengo la kuongeza wigo wa ufanisi katika utendaji. Wajumbe katika mafunzo hayo walipata Elimu ya Ushirika kwenye maeneo mbalimbali kama vile Dhana ya Ushirika, Utawala Bora na Maadili, Utatuzi wa Migogoro, Masuala ya Kodi, Uandaaji na Udhibiti wa bajeti, Masuala ya Rushwa kwenye Vyama vya Ushirika, huduma kwa wanachama, uandaaji wa makisio, ukomo wa madeni, kupanga mpango mkakati, ununuzi na Itifaki.



*Wajumbe wa Bodi za Vyama vya Ushirika Ushirika vya Wakulima wa Miwa kutoka Kagera, Mtibwa, Kilosa, Kilombero na Mbigiri (Magore) wakiapa kiapo cha Uadilifu kabla ya kuanza majukumu yao ya kazi katika Vyama vyao vya Ushirika*



*Wajumbe wapya wa Bodi za Vyama vya Ushirika toka Halmashauri ya Korogwe DC, Korogwe Mji na Handeni DC wakila kiapo cha Uadilifu Mkoani Tanga*

# MASWALI NA MAJIBU KUHUSU CHAGUZI ZA VIONGOZI WA VYAMA VYA USHIRIKA

## 1. JE, NI VYAMA VIPI VINAVYOHUSIKA NA UCHAGUZI?

Vyama vinavyohusika katika uchaguzi wa Viongozi ni Vyama vyote vya Ushirika ambavyo uongozi wake umekaa madarakani kwa muda wa Miaka mitatu.

Vyama hivyo ni pamoja na Vyama vya ushirika vya Msingi, Vyama vikuu, Miradi ya pamoja ya Ushirika na Ubia wa Vyama vya Ushirika na Shirikisho ambavyo kimsingi wapo ndani ya mwaka wa tatu tangu walipofanya uchaguzi.

## 2. WAGOMBEA UONGOZI KWENYE VYAMA VYA USHIRIKA WANATAKIWA KUWA NA SIFA ZIPI?

I.) Awe amekamilisha kulipa Hisa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na masharti ya chama husika,

II.) Awe anashiriki kikamilifu katika shughuli za chama,

III.) Awe na angalau elimu ya sekondari itakayomwezesha kutekeleza majukumu atakayokabidhiwa,

IV.) Awe na rekodi nzuri ya uaminifu wa kiwango cha juu,

V.) Asiwe anafanya biashara inayofanana na ya chama anachogombea,

VI.) Awe amehudhuria angalau mikutano mikuu ya mwaka miwili isipokuwa kama ni kwa Bodi ya kwanza tangu kuandikishwa.

VII.) Awe na Fungamanisho linalompa sifa ya kuwa Mwanachama

VIII.) Awe hajahukumiwa kwa kosa lolote la jinai na hajawahi kuhukumiwa kifungo kinachozidi miezi sita.

IX.) Awe hajasababisha hasara kwenye Chama chochote cha Ushirika,

X.) Asiwe na mikopo ya chama iliyopitisha muda wa kurejeshwa kulingana na mkataba wa mkopo husika

## 3. JE, VIONGOZI WA KISIASA AU SERIKALI WANARUHUSIWA KUGOMBEA UONGOZI KATIKA CHAMA CHA USHIRIKA?

**HAPANA**

Kifungu cha 132 (1) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 kinawazuia Wanachama wa Vyama vya Ushirika ambao ni Viongozi wa siasa au viongozi wa Serikali wenye vyeo vinavyoainishwa kwenye kifungu 132(4) kutokuwa viongozi wa Vyama vya Ushirika wakati wakiwa katika nyadhifa zao za kisiasa au Serikalini isipokuwa kama mwombaji anaomba uongozi katika chama cha kazini kwake au chama kilichoanzishwa ndani ya chama chake cha siasa.

## 4. NINI MAJUKUMU YA MWANACHAMA KATIKA MCHAKATO WA UCHAGUZI?

Majukumu ya mwanachama katika mchakato wa kupata viongozi ni pamoja na:

- Kuomba kuwa kiongozi kama anaona anazo sifa za kuwa kiongozi,

***Inaendelea ukurasa wa 25***


# MCHANGO WA VYAMA VYA USHIRIKA WA NYUMBA KUFIKIA AZMA YA NYUMBA KWA WOTE

Sote tunatambua kwamba nyumba bora ni moja ya mahitaji muhimu kwa binadamu ili kumpatia hifadhi yenye usalama. Kuishi katika nyumba bora huchangia utendaji kazi wenye tija na kutoa mchango katika shughuli za uzalishaji mali. Nyumba ni mojawapo ya mambo ya msingi katika kuwezesha ukuaji wa maendeleo ya jamii na uchumi kwa ujumla (JMT, 2013). Hata hivyo, ongezeko la watu duniani limesababisha ongezeko la uhitaji wa nyumba vijijini na mijini. Hata hivyo, tatizo limekuwa kubwa zaidi sehemu za mijini hasa katika nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania.

Nchini Tanzania, karibu asilimia 98 ya nyumba za makazi huzalishwa na watu binafsi kwa kutumia akiba zao wenyewe na kujengwa kidogo kidogo katika maeneo rasmi na yasiyo rasmi ambapo kati ya asilimia 50 hadi 70 ya wakazi wa mijini wanaishi ambapo muda wa ujenzi unakadiriwa kufikia wastani wa miaka 5 hadi10 hadi kukamilika.

## Makadirio ya Ongezeko la Idadi ya Watuna Uhitaji wa Makazi Bora

Utafiti uliofanywa na Pienaar, (2020) unaonyesha kuwa, Tanzania inakadiriwa kuwa na idadi ya watu milioni 60 ifikapo mwishoni mwa mwaka 2020. Kiwango cha ukuaji ni zaidi ya 3% kwa mwaka inakadiriwa kuwa, kufikia mwaka 2030 idadi ya watu nchini Tanzania itaongezeka na kufikia zaidi ya watu milioni 79. Na ifikapo mwaka 2050, inakadiriwa kuwa idadi ya watu itafikia zaidi ya milioni 129. Ongezeko hili linaenda sambamba na ukuaji wa mahitaji ya makazi / Nyumba




*Makadirio ya Idadi ya Watu Mijini*

## Makadirio ya Ongezeko la Idadi ya Kaya

Mwaka 2018, Tanzania ilikuwa na kaya milioni 12.3. Kati ya hizo kaya milioni 8.2 (66%) zilikuwa za Vijijini na milioni 4.2 (34%) zilikuwa za mijini. Kutokana na tafiti hiyo ya Pienaar (2020), inakadiriwa kuwa katika kipindi cha miaka 5 ijayo, idadi ya Kaya katika maeneo ya vijijini itaongezeka kwa kaya 255,000 kwa mwaka na kaya za mijini 1,300,000 kwa kila mwaka. Kutokana na makadirio haya, idadi ya kaya inaweza kuongezeka kama ifuatavyo:-




***Ongezeko la Idadi ya Kaya***

Hivyo, ni dhahili kuwa ongezeko la idadi ya kaya, linahitaji liende sambasamba na ujenzi wa nyumba zenye ubora na zenye bei nafuu zaidi ili kukidhi mahitaji ya makazi (Mijini na Vijijini).

## Makazi Bora Kupitia Vyama vya Ushirika wa Nyumba

Vyama vya ushirika wa nyumba vimekuwa ni mojawapo ya njia zinazotumika kuwezesha watu, hasa wa kipato cha chini, kupata makazi bora sehemu mbalimbali ulimwenguni kote. Vyama vya ushirika vinaweza kutumika kama njia katika upangaji na uendelezaji wa makazi katika nyanja mbalimbali. Dhana ya Ushirika ambayo inazingatia watu kusaidiana na kujisaidia, hivyo ushirika wa nyumba hutoa huduma kwa wanachama wao ikiwemo kuwasaidia kupata mikopo ya nyumba, kupata viwanja na huduma za mipango ya miji kwa njia rahisi.



***Baadhi ya nyumba za Wanachama wa Chama cha Ushirika wa nyumba Sejeseje kilichopo Jijini Dodoma***

## Je, Ushirika wa Nyumba ukoje?

Ushirika wa nyumba huchukua sura tofauti tofauti katika mataifa mbalimbali. Hivyo, ni vigumu kuwa na tafsiri moja juu ya Ushirika wa Nyumba. Brockway (2018) alitafsiri Ushirika wa Nyumba kama: Asasi ya Ushirika inayomiliki au kukodisha nyumba za makazi kwa kusudi la kumilikisha au kutumiwa na wanachama wake ambapo dhumuni lake kuu ni kusaidia wanachama wake kupata makazi kwa gharama nafuu.

Kwa ujumla, Ushirika wa Nyumba ni aina ya ushirika unaoundwa kushughulikia mipango ya ujenzi wa nyumba kwa wanachama wake (JMT, 2013). Pia tunaweza kusema kuwa Ushirika wa Nyumba ni taasisi iliyoandikishwa kwa mujibu wa sheria na kuundwa na watu ambao wanataka kufanya uendelezaji wa nyumba zao kutumia juhudi za pamoja.


## Vyama vya Ushirika wa Nyumba Nchini

Vyama vya ushirika wa nyumba hapa nchini, pamoja na kutambuliwa katika mihimili mbalimbali ya kisera kama vile; Sera ya Maendeleo ya Ushirika (2002), Sera ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000, bado havijapewa msukumo mkubwa ili kuwezesha wananchi wengi wa kipato cha chini kujiunga ili kupata makazi bora kwa bei nafuu.

Hadi kufikia Mwezi Oktoba, 2018 idadi ya Vyama vya Ushirika wa Nyumba nchini vilikuwa ni 16 tu. Mkoa wa Dar es Salaam ukiwa unaongoza kwa kuwa na vyama sita (6) ikifuatiwa na Mikoa ya Kagera na Mwanza ambavyo vilikuwa na vyama (2). Mikoa mingine ilikuwa na chama kimoja ikiwemo; Arusha, Dodoma, Tanga, Iringa na Mtwara.

## Vyama vya Ushirika wa Nyumba katika Nchi Mbalimbali

Ushirika wa nyumba ndilo kimbilio la watu wengi katika mataifa mbalimbali Duniani. Baadhi ya nchi sehemu kubwa ya nyumba ni za Vyama vya Ushirika wa nyumba. Mfano wa nchi hizo ni hizi hapa chini katika kielelezo.




***Ushirika wa Nyumba katika nchi mbalimbali***

## Umuhimu wa Vyama vya Ushirika wa Nyumba katika Mnyororo wa Thamani

Umuhimu wa Vyama vya Ushirika wa Nyumba unaonekana kutokana na huduma/bidhaa zinazotolewa na Vyama hivi. Vyama hivi huchukua sura tofauti tofauti katika nchi mbalimbali. Kutokana na utofauti huo, bidhaa zitolewazo huweza kutofautiana kutoka nchi moja hadi nyingine. Kwa ujumla, bidhaa hutolewa kwa hutegemea mahitaji ya wanachama, uwezo wa chama kifedha na hali ya kiuchumi inayotoa fursa kwa chama kutoa huduma bora na kwa wakati.

*Mwandishi wa Makala hii ni Afisa Programu Mwandamizi kutoka Taasisi ya Elimu Endelevu ya Ushirika ya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, Ofisi ya Dodoma.*

# MIFUMO YA KIMASOKO YAWANUFAISHA WAKULIMA WA MKOA WA RUVUMA NA KUWAWEZESHA KUPATA BILIONI 28.6

Wakulima wa mkoa wa Ruvuma wameendelea kunufaika na matumizi ya mifumo ya masoko katika uuzaji wa mazao yao na kuwawezeha kupata Shilingi Bilioni 28.6 katika msimu wa 2020/2021 kwenye mazao ya Ufuta, Soya na Mbaazi. Mazao haya yaliuzwa kupitia Ushirika kwa mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika Wilaya za Namtumbo, Tunduru, Songea, Mbinga na Nyasa.

Mauzo ya mazao hayo yalifanyika kupitia minada ya Sanduku iliyoendeshwa chini ya usimamizi wa Vyama vikuu vya TAMCU Ltd kwa Wilaya ya Tunduru na Chama Kikuu cha SONAMCU Ltd kwa Wilaya za Namtumbo, Songea, Mbinga na Nyasa.

**Uendeshaji wa Masoko ya Msimu wa 2020/2021**

Ukusanyaji wa mazao ya Wakulima ulifanyika kupitia Vyama vya Msingi 44 kwa Wilaya ya Namtumbo, Wilaya ya Songea vyama 6, Wilaya ya Mbinga vyama 2, wilaya ya Nyasa chama 1 na vyama 35 kwa Wilaya ya Tunduru. Hivyo kufanya jumla ya Vyama vya Ushirika vilivyoshiriki katika minada ya masoko ya mazao haya kwa msimu huu kufikia jumla ya 90 ikiwa vyama vya Msingi 88 na Vyama Vikuu 2.

## i. Ufuta

Jumla ya kilo zilizokusanywa na kuuzwa katika Msimu huu ni kilo **12,234,757** ambapo wakulima walilipwa kiasi cha shilingi **25,062,688,275.00**. Aidha, bei ya juu katika Msimu huu ilikua shilingi **2,408** na bei ya chini ilikua shilingi **1,300**. Minada yote ilifanyika kupitia Sanduku la wazi. Jumla ya Minada iliyofanyika ilikua 29 (10 ilifanyika Wilaya ya Tunduru na 19 Wilaya ya Namtumbo na Songea).

## ii. Soya

Jumla ya kilo zilizokusanywa na kuuzwa katika Msimu huu ni kilo **1,499,077** ambapo jumla ya mauzo ilifikia Shilingi **1,067,158,147.00** ikiwa ni kiasi kilicholipwa kwa Wakulima**.** Aidha, bei ya juu katika Msimu huu ilikua Shilingi **775** na bei ya chini ilikuwa Shilingi **693.**Jumla ya Minada iliyofanyika ilikuwa 9 kwa Wilaya za Songea na Namtumbo.

## iii. Mbaazi

Jumla ya kilo zilizokusanywa na kuuzwa katika Msimu huu ni kilo **4,260,777** ambapo jumla ya mauzo ilifikia Shilingi **2,585,676,632.00.** Aidha, bei ya, juu katika Msimu huu ilikuwaShilingi 790 na bei ya chini ilikua Shilingi 525. Jumla ya Minada iliyofanyika ilikuwa 10 (minada 4 ilifanyika Wilaya ya Tunduru na 6 Wilaya ya Namtumbo).

Pamoja na mafanikio yaliyojitokeza, mambo yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa:



*Mavuno ya zao la Ufuta*

i. Wakulima, vingozi wa kiserikali na wadau waendelee kuelimishwa na kuhamasishwa juu ya matumizi ya mifumo mbalimbali ya masoko ili kuongeza ufanisi na kuondoa changamoto zinazoweza kujitokeza;

ii. Wakulima waendelee kuhamasishwa kuongeza uzalishaji wa mazao unaozingatia ubora ili wazidi kunufaika na bei na kuvutia wanunuzi; na

iii. Halmashauri zinashauriwa kuunda timu za wataalam ya uhakiki wa Malipo ya wakulima (Payment Centres) ili ziweze kupitia usahihi wa miamala/orodha ya Malipo ya Wakulima kabla ya kuwasilisha benki kwa hatua za malipo.



***Soya ikiwa shambani***

## MASWALI NA MAJIBU KUHUSU CHAGUZI ZA VIONGOZI WA VYAMA VYA USHIRIKA (*Inatoka ukurasa wa 21*)

- Kuhamasisha wanachama wenzake wenye uwezo na sifa za kuwa viongozi kujaza fomu za kuomba uongozi,
- Kutoa taarifa kwa kamati ya uchaguzi juu ya mwanachama ambaye amejaza fomu lakini ana uhakika kuwa mwanachama huyo amekosa sifa za kuwa kiongozi.
- Kuhudhuria mkutano wa uchaguzi na kutumia haki yake ya kuchagua na kuchaguliwa.

### 5. WASIMAMIZI WA UCHAGUZI KWENYE VYAMA VYA USHIRIKA WANAPATIKANAJE?

Kwa mujibu wa kifungu cha 21 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika, Mrajis au mtu aliyemkaimisha madaraka atateua Wasimamizi wa uchaguzi kwa idadi atakayoona inafaa. Mrajis kwa kutumia Mamlaka hayo huwateua wasimamizi wa uchaguzi katika ngazi za Halmashauri na Mkoa.

### 6. CHAMA KINATAKIWA KUWA NA WAJUMBE WA BODI WANGAPI?

Kwa mujibu wa Sheria Na. 6 ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2013 idadi ya wajumbe wa Bodi watakaochaguliwa itatokana na masharti ya chama husika au kama itapendekezwa na wanachama na kuazimiwa katika Mkutano mkuu wa uchaguzi. Hata hivyo, Sheria inawataka vyama vya Ushirika kuwa na wajumbe wa Bodi wasiopungua watano (5) na wasizidi wajumbe tisa (9).

# WAKULIMA WA CHOROKO MWANZA WANUFAIKA NA MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA

***Mkoa wa Mwanza ni moja ya mikoa inayozalisha zao la Choroko kwa wingi nchini Tanzania. Katika mkoa huo Choroko huzalishwa katika Halmashauri za Kwimba, Magu, Misungwi na Sengerema.***

Msimu wa biashara ya Choroko mkoani Mwanza wa 2020/2021 ulianza tarehe 25/01/2021 ambapo ukusanyaji wa choroko ulianza. Kabla na baada ya kuanza kwa ununuzi huo tarehe 22/01/2021 na 27/01/2021 vilifanyika vikao vilivyohusisha wadau wanaohusika na usimamizi wa mfumo wa ununuzi wa choroko kupitia stakabadhi za ghala, lengo la vikao hivyo ni kuweka utaratibu mzuri wa kuhakikisha kila mdau anashiriki kikamilifu katika usimamizi na ufuatiliaji wa biashara ya Choroko kwa kutumia mfumo huo. Wadau waliohusika ni pamoja na Uongozi wa Mkoa wa Mwanza, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri, Wawakilishi wa wakulima wa Choroko, Soko la Bidhaa Tanzania (TMX), Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala, Viongozi wa Chama Kikuu cha Ushirika na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC).



***Viongozi wa Vyama vya Ushirika na wawakilishi wa wakulima wakielimishwa juu ya matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala***



*Mkulima akichambua Choroko kabla ya kuhifadhi katika vifungashio*

Hadi kufikia mwanzoni mwa mwezi Aprili, jumla ya minada 18 imefanyika kwa Halmashauri za Kwimba, Magu, Misungwi na Sengerema. Kupitia minada yote hiyo jumla ya **tani 3,475,886** ziliuzwa na kiasi cha **Tshs 5,185,495,358** kilikusanywa na kulipwa kwa wakulima.

Matumizi ya mfumo huu yanameleta faida mbalimbali kwa wadau kama ifuatavyo:

i. Kupatikana kwa malipo ya ushuru kwa wakati na hivyo kuongeza mapato ya Serikali na Ushirika kwa ujumla;

ii. Kuwepo kwa bei nzuri ya ununuzi: Katika mnada wa kwanza bei ilikuwa Shilingi 1,493 kwa kilo ukilinganisha na bei ya wananuzi binafsi ambayo ilikuwa ni kati ya Shilingi 900 hadi 1,000. Mnada wa pili bei ya mnada ilikuwa Shilingi 1,623 kwa kilo ikilinganishwa na bei ya Wanunuzi Binafsi ambayo ilikuwa ni kati ya Shilingi 1,000 hadi 1,200 kwa kilo na Mnada wa mwisho bei ya Mnada ilikuwa Shilingi 1,204 kwa kilo wakati wanunuzi binafsi bei ikiwa kati ya Shilingi 600 hadi Shilingi 800 kwa kilo;

iii. Mkulima kupata uzito sahihi wa mazao yake kutokana na matumizi ya vipimo sahihi vya Serikali (mizani iliyohakikiwa); na

iv. Upatikanaji wa takwimu sahihi za uzalishaji na mauzo ya Choroko.

*Limetolewa na*
**Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC)**
Mtaa wa Kuu,  S. L. P. 201, **DODOMA.**
Simu: +255 26  23 22456,  Telefax: +255 26 23 21973
B.Pepe: **ushirika@ushirika.go.tz** Tovuti: **www.ushirika.go.tz**

